MISINGI YA AZIMIO LA ARUSHA NA MAENDELEO YA TANZANIA

Katika Kikao chake cha Kawaida kilichofanyika mjini Zanzibar kuanzia tarehe 14/2/91 hadi tarehe 16/2/91 Halmashauri Kuu ya Taifa ilichukua maamuzi mazito kuhusu utekelezaji wa Azimio la Arusha - maamuzi ambayo uzito wake unalingana kabisa na hali ya kutangazwa kwa Azimio lenyewe mwaka 1967. Hivyo si jambo la kushangaza kuona kwamba watu wamekuwa na shauku ya kusikia kama maamuzi haya yanafuta Azimio la Arusha au la. Aidha, Vyuo vyetu vya Chama na Taasisi zingine ambazo zilikabidhiwa wadhifa wa kulifundisha Azimio na kutoa ufafanuzi wa mwelekeo wa siasa ya nchi yetu, vinategemea pia kupatiwa mwongozo na Chama kuhusu ufafanuzi wa maamuzi haya.

Kwa bahati nzuri, Mwenyekiti wa Chama amekwisha kutamka kwamba maamuzi haya hayafuti Azimio; bali yana lengo la kuliimarisha Azimio. Makala haya yanakusudia kutoa maoni ya mwandishi wa makala haya juu ya jinsi anavyoelewa yeye umaana wa maamuzi hayo na namna yanavyohusiana na utekelezaji wa Azimio la Arusha. Aidha, ni makusudio ya makala haya kuonyesha jinsi maamuzi haya yanavyoweza kusaidia kutekeleza lengo la Azimio la Arusha endapo wale ambao wamekabidhiwa madaraka ya kuliongoza Taifa hili - hasa katika nyanja za Uchumi - wana dhamira ya kweli ya kuwasaidia wananchi wote kwa jumla kushiriki katika kuendesha na kumiliki uchumi wa nchi hii. Kwani ni kweli kabisa kwamba ingawa siasa ya nchi hii ni nzuri na ina lengo dhahiri la kuwapa wananchi kauli ya kutawala uchumi wao, wengi wa viongozi waliokabidhiwa madaraka ya kusimamia vyombo muhimu vya uchumi, wametumia nafasi hizo kupotosha malengo ya Azimio la Arusha ili lisitekelezeke. Hivyo wamelihujumu Azimio la Arusha ili hatimaye watekeleze imani yao ya kibepari kwa kisingizio kwamba Ujamaa hauwezekani.

Kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba mbele ya viongozi wenye mawazo ya kibepari na ambao ndio wamesababisha baadhi ya mambo yetu kuzorota, watatafsiri maamuzi haya kama ni kuondoka katika misingi ya Azimio

.../2.

la Arusha na kwamba sasa wana uhuru wa kutekeleza wazi wazi yale yote ambayo walikuwa wanayafanya kisirisiri.

Makala haya yanakusudia kutoa ilani kwa viongozi kama hao na wengine ambao huenda wana mawazo hayo kwa kuonyesha kwamba kama tutatafsiri maamuzi muhimu yaliyotolewa Zanzibar kwamba ni leseni kwa sisi viongozi kujilimbikizia mali, basi tutafanikiwa kupotosha nia njema ya uongozi wa juu wa Chama wa kutaka Azimio la Arusha lidumishwe kwa kuliwezesha kutekelezwa kwa urahisi zaidi. Ili kutoa ufafanuzi huo, ni vizuri tukajikumbusha nini hasa lengo la Azimio la Arusha:-

Chimbuko hasa la Azimio la Arusha ni Imani ya Chama ambayo katika mambo ya uchumi imesisitiza juu ya umuhimu wa kuhakikisha:-

> "Kwamba raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vijavyo";

na

> "Kwamba ni wajibu wa Serikali ambayo ni watu wenyewe, kuingilia kati kwa vitendo maisha ya uchumi ya Taifa ili kuhakikisha ustawi wa raia wote na kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine au kikundi kimoja kunyonya kikundi kingine na kuzuia limbikizo la utajiri kufikia kiasi ambacho hakipatani na siasa ya watu wote kuwa sawa".
> (mkazo ni wa mwandishi).

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba msingi mkubwa wa Azimio ni "USAWA WA BINADAMU". Usawa wa binadamu unapatikana kama mambo matatu yafuatayo yanatendeka:-

(a) Kutokuwepo unyonyaji

(b) Njia kuu za uchumi zikitawaliwa na umma wa wakulima na wafanyakazi wenyewe.

(c) Kuwepo kwa demokrasi ya kweli - kwa maana kwamba "serikali iwe inachaguliwa na kuongozwa na wakulima na wafanyakazi wenyewe". Azimio la Arusha linasisitiza kuwa "Hakuna Ujamaa wa kweli pasipo Demokrasi ya kweli". (mkazo ni wa mwandishi).

Mambo haya matatu yakitimizwa, basi tutakuwa tumetekeleza vizuri matakwa ya Azimio kwa maana kwamba kile kinachopatikana kitagawanwa na wananchi wote kwa misingi ya usawa. La muhimu ni kwamba lazima tuwe na uongozi ambao unatambua umuhimu wa misingi hii na ambao unaamini pia kwamba misingi hii ni muhimu izingatiwe kila wakati. Aidha, uongozi sharti uwe na imani kwamba misingi hii inaweza kutekelezeka.

Kwa hiyo swali kubwa ni kwa vipi maamuzi ya Zanzibar yatasaidia utekelezaji wa misingi hiyo muhimu? Tutajaribu hapa chini kuelezea kwa kifupi maamuzi muhimu yaliyotolewa Zanzibar; athari zake na/au faida kwa Azimio na kwa jinsi gani yanaweza kuleta athari na/au faida; na namna gani tunaweza kuyapanua maamuzi hayo ili yalinufaishe vizuri zaidi Azimio. Pia makala haya yatazingatia matatizo yanayoweza kutokea kwa upanuzi huo. Mwisho, makala itatoa mapendekezo ambayo mwandishi wa makala haya angeomba ngazi za juu za Chama ziyafikirie. Tutazungumzia kila uamuzi peke yake kwa hatua zote tatu:-

1. <u>SUALA LA KUPANGISHA NYUMBA:</u>

Katika mambo yote yaliyoamuliwa Zanzibar hili ndilo lenye uzito zaidi katika kulisaidia Azimio au kulibomoa. Upangishaji wa nyumba ni kipengele ambacho ni rahisi kulibomoa Azimio kwa sababu ni njia moja ya vitega uchumi ambayo ingawa gharama za kuanzia ni kubwa, lakini mtu akiweza kujenga nyumba moja na kuipangisha ni rahisi sana yeye kujenga hata nyumba elfu moja zingine au zaidi. Kwa hiyo athari za kupangisha nyumba ni kubwa sana katika kudumisha ulimbikizaji wa mali kwa mtu mmoja; ingawa huduma yenyewe ya nyumba ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa lolote. Aidha, ingawa kwa mantiki hiyo hiyo, upangishaji wa nyumba una faida kubwa kwa uchumi kwa kuwaongezea watu mapato ambayo kwayo yanawawezesha kuweka akiba na vitega uchumi zaidi katika maeneo mengine ya uchumi, ni kweli pia kwamba kwa kufanya hivyo, ni rahisi sana kuleta tofauti kubwa katika mapato ya jamii na hivyo, kuwafanya wenye nyumba kuwa matajiri zaidi kuliko wapangaji wao. Kwa maana hiyo, upangishaji wa nyumba usipo-dhibitiwa vizuri, ni chanzo kikubwa cha unyonyaji na hivyo kinazuia ujenzi wa jamii ya watu walio sawa.

.../4.

Kwa hiyo suala muhimu ni namna gani unaweza kudhibiti hali hiyo? Kama Mwenyekiti alivyosema, madhumuni ya uamuzi huu ni kuwawezesha viongozi kujitegemea wenyewe wanapostaafu kwa kujijengea nyumba ambazo wataweza kuzilipia mikopo na matengenezo yake wakati wangali ni watumishi na wakaweza kuishi humo wamalizapo muda wao wa kazi. Aidha, kama nyumba ni nzuri na iko katika eneo au mji wenye wateja wengi, mapato kutokana na kodi yataweza pia kutoa salio ambalo linaweza kumsaidia mwenye nyumba kumudu gharama zake za maisha yake wakati akiendelea na utumishi - na pengine hata kujijengea nyumba nyingine ambamo yeye ataishi anapostaafu wakati nyingine ikimpatia chakula chake.

Lakini ni kweli pia kwamba kama halikudhibitiwa sawa sawa na kwa haki kwa wote, sharti hili linaweza kuwa ndicho chanzo kikubwa cha tofauti za mapato na maisha na hivyo ikatuwia vigumu sana kujenga jamii ya watu walio sawa. Ndiyo maana baadhi ya wananchi wametamka kwamba uamuzi huu ni njama za viongozi kulindana kwa kuhalalisha yale ambayo wamekuwa wakiyafanya kisirisiri. Kwani ni kweli kwamba sehemu kubwa ya viongozi wamekuwa na mali za namna hii!!

Kwa hiyo ni jambo la muhimu kwa Chama na Serikali kutilia maanani maoni hayo kama kweli tunataka kuwasaidia wananchi bila ya kuathiri msingi muhimu wa Azimio wa kutaka tujenge jamii ya watu walio sawa. Ziko njia nyingi za kudhibiti jambo hili na kuhakikisha kwamba mapato ya watu hayapitani sana kutokana na uamuzi huu. Kuu katika hizo ni kama zifuatazo:-

(a) Kudhititi utoaji wa viwanja. Halmashauri Kuu ya Taifa iliwahi kuamua jambo hili mwaka 1978 kwamba watu wasipatiwe viwanja zaidi ya kimoja katika miji kabla wengine hawajapata hata kiwanja kimoja. Lakini uamuzi huu pia ulikuwa na walakini; kwani haukutamka nini kifanyike kwa wale ambao tayari wana nyumba nyingi au viwanja vingi katika mji mmoja. Aidha, haikutamkwa kama kuna ubaya kwa mtu kuwa na nyumba katika kila mji wa nchi hii.

Kwa hiyo, kwa jumla uamuzi huu ulibakia katika makaratasi kwa sababu haukuzingatia matatizo yote ya utekelezaji. Hata uamuzi wa hivi sasa utapatwa na tatizo hilo kwa sababu njia za kuwadhibiti viongozi kuto kugeuza upangishaji wa nyumba kuwa ni biashara hazikufafanuliwa. Hivyo ni muhimu kwa watekelezaji kufanya ufafanuzi huo.

(b) Kurahisisha upatikanaji wa mikopo na viwanja. Ili kuhakikisha kwamba kila mwenye kutaka kujenga nyumba anawezeshwa kujenga angalau nyumba moja, Chama na Serikali sharti wahakikishe kuwa angalau kila mwenye kutaka kujenga anapatiwa mkopo kwa masharti nafuu ya kujenga nyumba yake ya kwanza na kwamba viwanja vinapatikana kwa urahisi. Suala la viwanja linaweza kutatuliwa kwa kuchanganya na udhibiti nambari (a) hapo juu. Lakini suala la mikopo linahitaji kuwako kwa sera nzuri ya uwekaji akiba na uwekezaji wa raslimali za mabenki. Sera ya namna hiyo siyo rahisi kupatikana chini ya udhibiti wa IMF na Benki ya dunia. Sera za mashirika haya kamwe hazitakuwa na maslahi kwa wanyonge. Kwa hiyo ni juu ya nchi husika kujizatiti vizuri sana katika kukabiliana na masuala ya ukwasi katika nchi na mwenendo wa mapato na bei ili kuhakikisha kwamba benki za nchi zinawanufaisha watu wote - na hasa wanyonge.

(c) Kuunda Makampuni na Mabenki ya Umma ya kujenga nyumba. Wazo hili kwa upande linalingana na wazo lililoko katika (b) hapo juu. Lakini hili lina mapana zaidi na linahusiana na uamuzi wa kuwaruhusu viongozi kuwa na hisa katika makampuni ya umma au makampuni ya kibepari ambamo wao ni wafanyakazi.

Katika Azimio la Arusha tulitamka kwamba njia kuu za uchumi zimilikiwe na wakulima na wafanyakazi ama kwa kupitia katika serikali yao au kwa kupitia katika vyama vyao vya ushirika. Kwa bahati mbaya sana, mwaka 1976 tulifuta Vyama Vikuu Vya Ushirika ambavyo ndivyo vilikuwa mikondo muhimu ya wananchi ya kuwekeza mali zao na vitega uchumi vyao. Kwa hiyo kwa kweli uamuzi huo ulipingana kidogo na Azimio. Kwa hali hiyo mkondo uliobakia kwa umma wote kumiliki uchumi wake uli-kuwa ni kwa kupitia serikali yao tu. Hicho ndicho kilikuwa chanzo cha serikali kulazimika kujitumbukiza katika miliki ya mashirika mengi ya uchumi; kazi ambayo ilikuwa ni kubwa kuliko uwezo wa serikali kifedha.

Hivyo ni jambo la kufurahisha kuona sasa tumetambua kosa hilo na tumevirudisha Vyama Vikuu Vya Ushirika. Hiyo ni hatua muhimu katika kuweka uchumi mikononi mwa wananchi; ingawa bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba vyama hivi vinakuwa kweli ni vyombo vya wananchi wenyewe. Aidha, lazima tuhakikishe kwamba hakuna senti ya mwananchi inapotea kutokana na ama uzembe au ubadhilifu wa watumishi wa vyombo hivi muhimu vya uchumi.

Lakini kuna njia nzuri zaidi ya kuweka uchumi mikononi mwa umma; nayo ni kuwashirikisha wananchi wenyewe ama mmoja mmoja; au kwa kupitia ushirika wao wa Akiba na Mikopo; au kwa vyote viwili kwa pamoja katika kununua hisa za kampuni na Mashirika ya umma na binafsi. Wakati umefika wa kuanzisha soko la hisa ambapo wananchi watakuwa na nafasi ya kushiriki moja kwa moja kwa kuuza hisa zao au kununua hisa mpya.

Kwa hiyo tunapozungumzia udhibiti wa ulimbikizajimali mikononi mwa watu wachache kwa sababu ya upangishaji wa nyumba, ni vizuri kuanza kuzungumzia kugeuza Benki ya Nyumba na Shirika la Taifa la Nyumba kuwa ni <u>Kampuni za Umma wote</u> kwa kuwauzia wananchi hisa moja kwa moja ili mapato kutokana na Benki hiyo na au Shirika la Nyumba yagawanywe kwa wale wote wenye hisa. <u>Hii ndiyo dhana inayotegemewa kuzaliwa na uamuzi wa Zanzibar kuhusu kuwauzia wafanyakazi hisa za kampuni za binafsi wana-zozitumikia, au kuuza hisa za mashirika ya umma kwa umma wote wa Watanzania pamoja na viongozi wa Chama na Serikali.</u> Aidha wakati

umewadia wa kutofautisha kati ya Kampuni ya serikali; Kampuni ya binafsi; na Kampuni ya Umma. Kampuni ya serikali iwe ni ile ambayo sehemu kubwa ya hisa zake zinashikwa na Serikali Kuu. Kwa mujibu wa kifungu cha 27(1) cha Sheria ya Makampuni sura 212, Kampuni ya binafsi ni ile ambayo wenye hisa hawazidi hamsini (50) na wenye hisa hawaruhusiwi kuziuza kwa watu wengine. Pia umma kwa jumla haurusiwi kununua hisa katika kampuni ya namna hiyo. Hii ina maana kwamba wakati wa Mkutano Mkuu wa kampuni ya binafsi, watu wote wenye hisa wanaweza kuhudhuria binafsi kuzumgumzia maslahi ya kampuni yao.

Lakini kampuni yoyote inayoundwa chini ya SURA 212 ya Sheria zetu ambayo wenye hisa wanazidi 50, inaitwa ni Kampuni ya Umma (Public Company). Kampuni ya namna hii inaruhusiwa kuuza hisa zake kwa umma na wenye hisa wanaruhusiwa kuziuza kwa mtu yeyote anayezihitaji. Aidha ili kuhakikisha kwamba wenye hisa wote wanajua kunatendeka nini kwa vile wanaweza hata kuwa watu 10,000 au zaidi, basi kampuni hii inalazimika kisheria kuchapisha katika magazeti mizania yake ya mwaka pamoja na Taarifa ya Faida na Hasara (publish in the newspapers its Balance Sheet and Profit and Loss Account). Kampuni ya namna hii kwa kweli haina tofauti sana na ushirika kwani watu wengi watakuwa na hisa chache chache tu. Na kwa kutegemea thamani ya hisa, inawezekana kabisa mtu asiwe na hisa zaidi ya kumi. Hivyo mtu mmoja peke yake hawezi kugeuza sera za kampuni.

Kwa hali hiyo, hii ndiyo njia moja pekee ambayo inaweza kusaidia kudhibiti watu wachache wasijilimbikizie mali wakati walio wengi ni maskini. Aidha hii ni moja ya njia kuu za kukusanya nguvu za wananchi katika kuendeleza uchumi wao. Miliki ya kampuni inaweza kubakia mikononi mwa watu wachache wenye ujuzi na ambao wana hisa kubwa zaidi kila mmoja kuliko watu wengine. Lakini watamiliki kampuni kwa faida ya umma wote wa wenye hisa. Hivyo hata mtu wa kawaida, ataweza kushiriki katika kuchangia maendeleo ya uchumi wa Taifa naye akaweza kupata faida kutokana na mchango wake. Kwa njia hiyo, tutaweza kutumia utaalamu wa mabepari kuwanufaisha wanyonge ambao ingawa si wajuzi lakini wana uwezo wa kuwekeza fedha yao kidogo katika kampuni za wajuzi wa biashara. Kwa hiyo tutaweza kuitumia elimu ya watu hao wachache kwa faida ya wote.

Njia moja ya kuhakikisha kwamba wananchi wenye kipato cha chini pia wanashiriki katika kuchangia uendelezaji wa shughuli za kiuchumi ni kuanzisha vyama vingi vya AKIBA NA MIKOPO. Vyama hivi vyenyewe vinaweza kuuziwa hisa kwa niaba ya wanachama wao au vinaweza kuwakopesha wanachama fedha ya kununulia hisa zao binafsi. Tatizo la kuwakopesha wanachama kujinunulia hisa zao binafsi ni moja; - yaani mwanachama anaweza akaziuza hisa zake kwa mtu mwingine na chama chake kisijue; na hivyo fedha ile ikatumika vibaya. Kwa hiyo njia nzuri ni kuhakikisha kwamba vyama vyenyewe vya Akiba na Mikopo ndivyo vinauziwa hisa hizo. Kwa msingi huo, hata vyama vya Akiba na Mikopo vya viongozi vinaweza kununua hisa katika kampuni ya binafsi kama vikipewa nafasi.

2. UUZAJI WA HISA KWA WAFANYAKAZI:

Jambo lingine lililoamuliwa Zanzibar ni ruhusa kwa wanachama wa CCM ambao wanafanya kazi katika kampuni za kibepari kuweza kununua hisa katika kampuni hizo. Aidha wafanyakazi wa mashirika ya umma na viongozi wa Chama na Serikali pia waliruhusiwa kununua hisa katika mashirika ya umma ili kuyaongezea mashirika hayo mitaji.

Hatua hii ni muhimu sana na kweli inaweza kuchangia sana katika maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Kusema kweli, hii ndio hatua ambayo ilitakiwa ichukuliwe katika kuwashirikisha wafanyakazi chini ya utaratibu wa uundaji wa mabaraza ya kazi wa mwaka 1970. Tukitaka wafanyakazi wa nchi hii wawe na kauli katika vyombo ambavyo wanavifanyia kazi ni lazima tuwaruhusu pia wao kuwa na hisa pale - hasa katika vyombo vya uchumi. Wenye kauli katika kampuni ya biashara ni wenye hisa. Kwa hiyo tukitaka wafanyakazi wa kampuni na mashirika ya biashara wawe na kauli ya kweli ni muhimu wawe na hisa katika kampuni na mashirika hayo. Kwa msingi huo, suala zima la ushirikishaji wafanyakazi katika kufikia maamuzi ya vyombo vya biashara wanavyovifanyia kazi lazima litazamwe kwa upya na kufanyiwa mageuzi.

Kama tulivyokwisha kugusia hapo juu, huu ndio wakati wa kutofautisha kati ya kampuni ya serikali na kampuni ya umma. Ingawa bado kuna umuhimu wa kuwa na mashirika ya kiserikali chini ya Public Corporations Act (1969), lakini siyo yale ya biashara. Mashirika

au kampuni zote za biashara - hata zile za serikali -inafaa ziundwe chini ya sheria ya Makampuni Sura ya 212 na Memoranda zao na Taratibu za kuziandikisha zitamke wazi wazi sehemu ya hisa ambayo itashikwa na wafanyakazi wa mahala pale au vyama vya Akiba na Mikopo vya wafanyakazi wa kampuni zingine ambazo zinahusiana na kampuni hiyo. Mathalani kama kampuni Tanzu moja ya TSA, NBC, TEXCO, NAFCO, SARUJI, au SUKARI n.k. inaanzishwa, basi sehemu kama asilimia 30 hivi ya hisa zake ziuziwe wafanyakazi wa kampuni ile na au wafanyakazi wa kampuni zingine za TSA, NDC, TEXCO, NAFCO, SARUJI au SUKARI n.k. kupitia vyama vyao vya Akiba na Mikopo. Wafanyakazi wa mashirika mama yenyewe pia waruhusiwe kupitia vyama vyao husika vya Akiba na Mikopo kununua hisa za kampuni yoyote Tanzu ya shirika hilo.

Hatua hiyo italeta faida kubwa tatu: Kwanza kabisa, kwa mara ya kwanza tutakuwa tumewashirikisha kikamilifu wafanyakazi katika shughuli za mahala pao pa kazi. Kwa vile na wao wana maslahi ya kweli kweli katika shughuli ya shirika au kampuni wanayoisimamia, uendeshaji na usimamizi wa kampuni hizi utafanyika kwa ufanisi zaidi. Aidha hata ulinzi wa mali ya kampuni hizi utakuwa madhubuti zaidi maana kampuni ni yao.

Pili tutajenga moyo wa kujiwekea akiba ambao kwa hivi sasa haupo kabisa. Watu wengi wanadhani Vyama vya Akiba na Mikopo ni vyama vya wanyonge tu. Hawaoni kwamba vyama hivi ni vya Watanzania wote kusaidiana. Na kweli vyama hivi ndio ufunguo wa kupunguza athari za mapato kupitana mno kwani ni chanzo kizuri cha mitaji kwa watu wenye kipato kidogo kwa ajili ya kufanyia kazi zao ndogo ndogo kwa vile masharti ya benki hawayawezi. Kwa hiyo vyama hivi vitazamwe kama ni mkondo mzuri wa wenye mapato makubwa kuwasaidia wanyonge ambao ni wanachama. Kwa msingi wa vyama hivi kutumiwa kama chombo cha kununulia hisa katika kampuni mbalimbali, hata wakubwa wataona umuhimu wake na wao wenyewe watajihusisha kikamilifu katika miliki yake. Na kwa kweli kama tukifanikiwa kuuza hisa kupitia Vyama Vya Akiba na Mikopo lingekuwa jambo jema zaidi kwani ni la kijamaa sana.

.../10.

Tatu kwa kuwahusisha wafanyakazi moja kwa moja katika miliki ya hisa za mashirika au kampuni tutaipunguzia serikali mzigo wa kutegemea kodi za wananchi au misaada kutoka nje. Vile vile tutapunguza urasimu kwani kampuni au mashirika haya yatajitegemea katika fedha na katika utendaji wao wa kazi. Huku ndiko kujitegemea kwa kweli.

Lakini hatua hii iwe ni ya mwanzo tu. Hatimaye, sharti tuunde soko la hisa (Capital Market or Stock Exchange) ambapo hisa za kampuni mbalimbali zitaweza kuuzwa na kununuliwa na watu; vyama vya ushirika; vyama vya Akiba na Mikopo; Mashirika; na kampuni mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Wakati huo ndipo tutahitajika pia kupanua tafsiri ya aina ya kampuni na mashirika mbalimbali kati ya kampuni au shirika la serikali; kampuni au shirika la umma chini ya Sheria ya Makampuni Sura 212 kwa maana kwamba kampuni au shirika hilo lina wenye hisa zaidi ya watu 50 na wenye hisa wanaruhusiwa kuziuza au kuzinunua hisa hizo katika soko la hisa; na mwisho kampuni au shirika la binafsi chini ya Sura 212 ya sheria kwa maana kwamba wenye hisa si zaidi ya 50 na hawaruhusiwi kuziuza katika soko la hisa, na wala umma hauruhusiwi kununua hisa katika kampuni au shirika hilo. Kwa njia hiyo <u>tutaweza kupanua zaidi uhuru wa wananchi na hata wanachama na viongozi wa kuwa na hisa katika Mashirika ya Umma ambayo wala si mali ya serikali bali ni mali ya wananchi wenyewe wakinunua hisa kila mmoja au kupitia katika Vyama vyao vya ushirika.</u> Kampuni za Umma za namna hiyo ya pili ndizo zinazoendesha uchumi wa dunia leo. Hatua hiyo ikifikiwa, itawezekana pia kujiwekea utaratibu kwamba kampuni ya binafsi ambayo raslimali au mauzo yake yanavuka kiwango fulani ambacho kitaamuliwa nyakati mbali mbali, itabidi igeuzwe kuwa Kampuni ya Umma na hisa zake ziuzwe na kununuliwa katika soko la hisa. Hatua hii inaweza kuwa lazima ili kuzuia watu wachache kutawala uchumi wa nchi bila kushirikisha wananchi wote ambao wangependa kushiriki katika biashara ile.

<u>Hapa ni vizuri kusisitiza kwamba suala la kujenga usawa na kupunguza tofauti za mapato kati ya watu ni la muhimu sana hata kama si kwa sababu za kijamaa. Kwani ni kweli kabisa kwamba kama viongozi</u>

watatumia mwanya wa maamuzi ya Zanzibar kujilimbikizia mali bila kujali maslahi ya raia walio wengi, hali hiyo itatuletea matatizo makubwa sana na hatimaye kutuangamiza.

Kwa msingi huu, ni vizuri kutamka hapa wazi wazi kwamba, ni jambo la kufa au kupona kuhakikisha kwamba Kampuni zote za Serikali ambazo tunataka kuziuza kwa watu zisiuzwe kisirisiri kwa wafanyabiashara wachache. Badala yake kampuni hizo ziwe ni chanzo cha kampuni za umma chini ya Sura Na.212 inayohusu uundaji wa kampuni na uuzaji wa hisa zake utangazwe hadharani. Vinginevyo, kampuni hizo ziuzwe kwa wafanyakazi na viongozi wa Chama na Serikali ambao kwa muda mrefu hawajapata nafasi ya kujiwekezea fedha katika vitega uchumi. LAKINI ITAKUWA BUSARA ZAIDI KUZIFANYA NI KAMPUNI ZA UMMA WOTE NA WANANCHI WOTE WAKARUHUSIWA KUNUNUA HISA HUMO.

3. **MTU KUPOKEA MISHAHARA MIWILI:**

Azimio hili ni zuri lakini lina athari zake. Ni zuri kama tutaweza kudhibiti watu na kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao za siku mahala pao pa kazi. Pia ni zuri mathalani kwa watu waliostaafu ambao hapo nyuma watu hawa wakiajiriwa kimkataba wamekuwa hawaruhusiwi kupata pensheni zao. Sasa itawezekana kuwatumia watu hawa kimkataba wakati papo hapo wakijipatia pensheni zao; jambo ambalo ni dhahiri litaweza kuwaongezea mapato yao na hivyo wakaweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Lakini ziko athari kubwa sana kama udhibiti wa utendaji kazi wa watumishi - hasa katika ofisi za serikali na mashirika ya serikali - hautakuwa mzuri. Iko hatari kwamba watu watafika kazini na kuweka saini ya kufika na mara wakatoka kwenda kufanya kibarua mahali pengine.

Kwa hiyo kuna umuhimu wa kuweka taratibu nzuri za kulitekeleza tamshi hili. Vinginevyo umma utakula hasara wakati watu wachache binafsi wanajinufaisha kwa kupata mishahara bila ya kufanya kazi. Aidha, iko haja ya kuitazama sheria inayohusu ajira ambayo inamkataza mtu kuajiriwa katika sehemu mbili. Hii wala si sheria ya Tanzania peke yake. Hata nchi za kibepari zina sheria kama hiyo kwa sababu ya matatizo yanayoweza kutokea katika kuwadhibiti watumishi.

.../12.

4. <u>KUHUSU KUFANYA BIASHARA AU KULIMA:</u>

Azimio hili kwa kweli halikuwa linawabana wanachama wa kawaida bali liliwabana sana viongozi. Wanachama wa kawaida kwa kweli wamekuwa wakifanya biashara na kulima mashamba makubwa; kwani hata Azimio kwa kweli halikuwazuia. Maana halisi ya mtu kuto kupata mishahara miwili ni kwamba huwezi kutumikia mabwana wawili. Kwa maana hiyo, msingi wa Azimio la Arusha ulikuwa kwamba mtu achague kuwa kiongozi wa umma au kuwa kiongozi wa miradi yake. Kwa msingi huo, wanachama wengi wamekuwa wakifanya kazi za miradi yao badala ya kuwa viongozi wa Chama au Serikali.

Hivyo uamuzi huu wa Zanzibar kwa kweli unawahusu viongozi wa Chama na Serikali. Kwa hiyo pamoja na umuhimu wa kuwapa nafasi ya kujiongezea mapato yao ili waweze kumudu gharama za maisha yao, lakini kuna umuhimu wa kuweka kikomo kwa viongozi. Ukiacha upangishaji wa nyumba ambao athari zake na udhibiti wake tumekwisha kuzungumzia hapo juu, siyo rahisi kwa kiongozi wa Chama na Serikali kuwa na mradi mkubwa au miradi midogo midogo mingi bila kuathiri ufanisi wake wa kazi kama hatakuwa na wasaidizi wa kuaminika.

Kwa hiyo kiutekelezaji iko haja ya kufanya ufafanuzi hapa. Ukweli wa mambo ni kwamba siyo rahisi kutokuwa na wasaidizi. Hivyo lingekuwa jambo jema kutambua ukweli kwamba viongozi wengi wenye miradi wana wasaidizi. Hata kama wasaidizi hao ni jamaa za viongozi hao lakini nao wanahitaji kupatiwa mishahara na wanahitaji kusimamiwa. Kwa hiyo la msingi lingekuwa mtu aruhusiwe wasaidizi wangapi ili mradi wake tuuite ni mdogo? Aidha hii ni nafasi ya kulegeza sharti linalounganisha uongozi kati ya mke na mume. Ingefaa kusema kwamba mmoja wao angeweza kusimamia miradi yao; ili mradi mtu asifanye kazi mbili kwa wakati mmoja.

Lakini kwa mwanachama ambaye si kiongozi wa shughuli za Chama na au za serikali, hatuna sababu kabisa ya kumwekea mipaka. La muhimu afuate sheria za nchi kikamilifu. Tena tunamtegemea mwanachama safi wa CCM awe ni mfano wa kuigwa katika kuwashirikisha wenzake - yaani wafanyakazi wake - katika miliki ya mali yake. Tukisema hivyo hatuna maana kwamba Chama na Serikali waache kuingilia kati kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanapatiwa haki zao kila mahala pa kazi.

.../13..

<u>MWISHO:</u>

Mwisho inapendekezwa kwamba:-

(a) Suala la upangishaji wa nyumba lifanyiwe ufafanuzi zaidi. Dalili zimeanza kuonekana kwa viongozi kuanza kuhodhi viwanja ili wajinufaishe. Hii ni hatari. Itatuletea matatizo makubwa. Kwa maoni ya mwandishi wa makala haya, inafaa hatua za haraka zichukuliwe kugeuza Benki ya Nyumba na Shirika la Nyumba (NHC) kuwa kampuni za Umma wote. <u>Watu wahamasishwe kujiunga katika Vyama vya AKIBA NA MIKOPO ambavyo vingeshauriwa kununua hisa katika Benki ya Nyumba ambayo pia itafaa kuruhusiwa kuanza shughuli za biashara ya kibenki.</u> Pia watu waruhusiwe kununua hisa binafsi katika benki hiyo.

Kadhalika, Shirika la Nyumba (NHC) ligeuzwe mara moja kuwa Kampuni ya Umma chini ya SURA Na.212 ya Sheria na watu waruhusiwe kununua hisa katika shirika hili ama wao wenyewe binafsi au kwa kupitia Vyama vyao vya AKIBA NA MIKOPO au Vyama vya Ushirika mwingine. Shirika hili lipanue shughuli zake na kuanza kujenga majengo makubwa ya kisasa ambayo kwayo mengine yangeliweza pia kuundwa kama Kampuni Tanzu zinazojitegemea na zikawa na wahisa binafsi wa ndani na nje ili mradi wahisa wa ndani wawe na hisa zisizopungua aslimia 51 au 60. Aidha shirika hili lingeweza pia kusaidia kuwakomboa watu wa Kariakoo; ILala; Temeke; Tandika; Buguruni; Mbagala; Magomeni ; Mwananyamala; Manzese, Mabibo; Kinondoni nakadhalika kwa kuthamini nyumba zao na kuzigeuza hisa katika shirika la nyumba. Baada ya kufanya hivyo, nyumba zao zinaweza zikabomolewa na kujenga badala yake majengo makubwa

.../14.

ambamo kila mmoja waliyebomolea nyumba yake atapewa "FLAT MOJA" ambayo atailipia. Sehemu zinazobakia zitakuwa mali ya Shirika au Kampuni husika ambamo na wao tayari watakuwa na hisa. LAZIMA TUKATAE TABIA YA KUWANUNUA WANYONGE NA KUWAHAMISHIA PEMBEZONI MWA MJI. Watu hawa wanahitaji kuendelezwa. Anayeweza kutetea maslahi yao ni Chama na Serikali. Na ili viongozi wachache wasijitajirishe kwa kujigawia viwanja vyote vya miji yetu, lazima tuunde chombo cha Umma wote ambacho ni cha wote lakini hakiendeshwi na serikali. Wakubwa wenye ujuzi wa mambo haya wanaweza wakaruhusiwa kuwa na hisa hadi aslimia kumi nao wakakabidhiwa madaraka ya kukiendesha. Lakini katu nyumba hizi zisiwe zao peke yao.

Suala hili ni muhimu sana na hatuwezi kulipa mkazo zaidi ya kusema kwamba hili ndilo suala ambalo litaamua kama nchi hii itaendelea kuwa ya amani au la. Wananchi wa nchi hii wamelielewa sana Azimio la Arusha na uzuri wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Watu wachache wakitumia vyeo vyao au nafasi zao katika jamii kujilimbikizia mali, tutaleta matatizo makubwa sana.

(b) Kuhusu ununuzi wa HISA katika Kampuni za kibepari na za umma pia ni suala la kufa au kupona. Njia pekee ya kuhakikisha kwamba na wanyonge nao wanashirikishwa ni kuanza haraka kufanya mambo yafuatayo:

(i) Kwanza suala la kuuza hisa lisingojee hisani ya mabepari. Chama na Serikali lazima kuamua kwamba hili sasa ni suala

la kisera. Kwa hiyo taratibu ziundwe za kupanua Waraka wa Rais wa mwaka 1970 kuhusu ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi ili katika vyombo vya kiuchumi, njia kuu ya kuwashirikisha iwe ni kuwapa fursa ya kuwa na hisa zisizopungua aslimia 30 mahala pao pa kazi. Aidha JUWATA sharti waone hii ndiyo kazi yao kubwa ya kutetea maslahi ya wafanyakazi. Ila suala hili lazima lisimamiwe vizuri. Iko hatari kwa mabepari kuwauzia wafanyakazi hisa za kampuni mfilisi halafu wao wakatoroka.

Ili kuhakikisha kwamba serikali ina nia njema juu ya jambo hili, yenyewe iwe ya kwanza kuwapa wafanyakazi wake hisa katika kampuni na Mashirika yake. Hapa tujitahadhari na vishawishi vya mabepari kwamba kwa kufanya hivyo tutazuia wawekezaji mali kutoka nje. Kama kwa kufanya hivyo tutaongeza uwekezaji mali wa Watanzania wenyewe ambayo ndiyo nia yetu hasa, basi tutafanikiwa sana kujenga uchumi unaojitegemea. Aidha watu wa kutoka nje wanajali zaid faida kuliko uhuru wa kuwa peke yao katika kampuni. Isitoshe, ni nchi gani duniani imeachia watu wa nje wajifanyie wanavyotaka? Tusiwaonee haya mabepari. Lazima tuhakikishe kwamba uwekezaji mali kweli una maslahi kwa wananchi wote na si kwa viongozi wachache.

(ii) Chama na Serikali waone ni jukumu lao kuanza kwa makusudi kabisa kuwahamasisha wananchi na hasa wafanyakazi kuanzisha mahala pao pa kazi Vyama vya AKIBA NA MIKOPO na kuhakikisha kwamba vyama hivyo vinaanzishwa kwa utaratibu

mzuri na kwamba hakuna senti ya mwanachama inayopotea. Vyama hivi ndivyo hasa viwe mkondo wa ununuzi wa hisa katika kampuni za umma na za kibepari. Kwa hiyo vyama hivi vitaweza kuteua wakurugenzi wao katika kampuni ya kibepari bila kuathiri Azimio la Arusha. Vinginevyo, itakuwa kinyume cha mambo (contradiction) wala si busara kuwaambia wafanyakazi wawe na hisa katika kampuni ya kibepari bila ya wao kuwa na uwakilishi katika Bodi ya Menejimenti.

Hapa ni vizuri tukawa macho kwamba si mabepari wote watalipenda tamshi hili. Lakini ni lazima wafanyakazi wanufaike kutokana na jasho lao. Hivyo inafaa Chama na Serikali kusimamia kikamilifu jambo hili; na njia pekee ya kuhakikisha kwamba linatekelezwa ni kuunda kwa makusudi Vyama vya Kuweka na Kukopa, au kwa jina lingine Vyama vya AKIBA NA MIKOPO.

(iii) Taratibu ziwekwe za kugeuza Kampuni za serikali zinazofanya faida na zile zenye uwezo wa kufanya faida kuwa Kampuni za Umma wote kwa mujibu wa SURA YA 212 ya Sheria za Tanzania na watu wote pamoja na viongozi wa Chama na Serikali waruhusiwe kununua hisa katika kampuni hizo. Aidha ili kuhakikisha kwamba shughuli hii baadaye inapanuliwa na kuhusisha Kampuni za binafsi, taratibu ziwekwe haraka za kuanzisha soko la hisa (Capital Market) ili kazi hii iweze kufanyika kwa ufanisi.

Utaratibu huu unaweza kuanza mara moja na Benki ya Taifa ya Biashara; Benki ya Nyumba ambayo ingeruhusiwa pia kufanya biashara ya

kawaida ya kibenki; Benki ya Maendeleo Vijijini; Shirika la Nyumba; Kampuni ya Bia; Kampuni ya Sigara; Bima ya Taifa; Mamlaka ya Mkonge Tanzania na Kampuni zake Tanzu kama Ngomeni Kamba, Mazulia; baadhi ya mashamba n.k.; Benki ya Rasilimali ambayo pia ingeruhusiwa kufanya biashara ya kawaida ya kibenki; Kampuni ya Viatu; Kampuni ya Sabuni (FOMA); na kadhalika; Mashirika haya yangelitosha kwa kuanzia. Ili mradi, nia ni kuweka uchumi mikononi mwa wananchi wenyewe - wakulima na wafanyakazi wa Tanzania. Watu wa nje wanaweza wakakaribishwa pia lakini wawe na hisa chache (yaani wawe "minority"). Aidha, ni muhimu kuzingatia taratibu za P.T.A. ambazo zinasisitiza kwamba Kampuni inayonufaika na soko la P.T.A. sharti imilikiwe na raia wa nchi inayohusika kwa aslimia 51 ya hisa au zaidi.

(c) kuhusu watu kupata mishahara miwili. Suala hili pia linahitaji ufafanuzi zaidi hasa kuhusu namna ya kulidhibiti. Ingelifaa mifano rasmi ikatolewa juu ya namna ya kuiruhusu au kutoiruhusu hiyo mishahara miwili.

(d) Kuhusu biashara na kilimo, iko haja ya kufafanua tofauti kati ya Mwanachama wa kawaida na Kiongozi wa Chama na Serikali. Hivi sasa watu wamechanganyikiwa. Wanaliona hili kama ni njia ya kuhalalisha tu mambo ambayo baadhi ya viongozi wamekuwa wakiyafanya. Lakini hata kama hivyo ndivyo, ni vizuri tukasema wazi wazi tunahalalisha nini na bado tunakataza nini? LAZIMA TUKUMBUKE KWAMBA MSINGI MKUBWA WA AZIMIO LA ARUSHA NI USAWA WA WATU. Kwa hiyo ni muhimu tujihadhari na ulimbikizaji wa mali ambao utakiuka azima hiyo.

(e) Mwisho, inapendekezwa kwamba kama itakubalika kwamba ufafanuzi huu ni mzuri na unatakiwa, basi ni vizuri ikaandaliwa rasmi mada au hotuba ambayo kwa makusudi kabisa, Mwenyekiti wa Chama angeliitoa mbele ya waalimu wote wa Chuo Kikuu cha Chama KIvukoni na vyuo vyake vya Kanda; wakiwepo na viongozi wa Taasisi zingine zinazofundisha masomo ya Maendeleo, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam na Chuo Kikuu cha Sokoine; Chuo cha Ushirika Moshi; Chuo cha Maendeleo Vijijini, Dodoma; na waalimu wa siasa katika Vyuo vingine na shule za Sekondari.

Ufafanuzi huo ni muhimu sana hasa kwa hawa ambao jukumu lao ni kuwaelewesha watu wengine juu ya siasa ya nchi. Aidha, tutaweza kutumia nafasi hiyo pia kukaribisha maoni yao juu ya ufafanuzi huu na mwingine katika kulitekeleza vizuri zaidi Azimio la Arusha. Hivyo tutaonyesha wazi wazi kwamba Halmashauri Kuu ya Taifa haikufunga milango kwa wanachama kutoa maoni yao pale ambapo wanaona maamuzi ya Halmashauri Kuu yanawalakini.

**MATOKEO:**

Matokeo ya Uamuzi huu wa Zanzibar ni kwamba sasa Chama kinaweza kuamua pia kwamba viongozi wa Chama hasa katika ngazi ya wenyeviti na Kamati zake uwe ni wa kujitolea kama wakati wa mwanzo wa TANU NA AFRO. Watu ambao watatakiwa kulipwa ni wale watendaji tu wa Chama. Aidha, hatimaye, hata Makatibu wangeliweza kuwa ni watu wa kujitolea tu maana watakuwa tayari na shughuli zao ambazo zinawapatia mapato mazuri zaidi.

Hili pia ni jambo ambalo linafaa kufikiriwa ili ikiwezekana kuanzia uchaguzi wa 1992 ijulikane wazi wazi kuwa viongozi wakuu wa ngazi zote hawatalipwa mishahara isipokuwa posho tu wanapokuwa katika shughuli za Chama nje ya sehemu zao wanapoishi. Hii itasaidia kupunguza sana

.../19.

gharama za Chama. Secretariat zinaweza kuwako kama Kamati za Utendaji na Makatibu wa Idara wakawepo. Lakini lazima wawe na kazi zao zingine na hawatalipwa mishahara na Chama. Ili kupunguza gharama za vikao, Chama kiwe na utaratibu wa kuwaweka watu katika Kamati za Utendaji ambao hawatakigharimu sana Chama katika kuwasafirisha kuhudhuria vikao.

Haya yanaweza kuwa ni matokeo mazuri ya Maamuzi ya Zanzibar.

I. M. Kaduma
KATIBU WA CCM (Taasisi)
MAMLAKA YA MKONGE TANZANIA

Tanga,
Machi, 1991.